

JUMANNE JUNI 30, 2009

Fedha alizoahidi Bush ziko pale pale - JK

Na John Nditi, Morogoro

SERIKALI imewahakikishia Watanzania kuwa fedha zote ilizoahidiwa na Marekani dola milioni 800 kwa ajili ya miradi mitatu mikubwa, zitaendelea kutolewa kama ilivyopangwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Rais Jakaya Kikwete juzi, wakati akihutubia wananchi wa tarafa ya Matombo, kuhusu utekelezaji wa mradi wa umeme katika tarafa za Mkuyuni na Matombo kupitia mpango wa fedha kutoka Serikali ya Marekani.

Rais aliwaondolea hofu juu ya upatikanaji wa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kijamii na kiuchumi, baada ya kusikiliza kilio cha wananchi wa tarafa hiyo juu ya kukosekana kwa huduma muhimu ya maji, afya na umeme kupitia Mbunge wa Jimbo hilo, Hamza Mwenegochi na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mtamba, Ferdinand Sigara.

"Fedha tuliyoahidiwa na Rais wa zamani wa Marekani, George W. Bush, kiasi cha dola milioni 800 zipo na Rais wa sasa Barack Obama ameruhakikishia kuwa fedha zote zilizopangwa kutolewa na serikali, zitatolewa kama ilivyopangwa," alisema Rais na kuongeza:

Serikali ya Rais Obama kama ingeweza kutekeleza. Lakini bahafi nzuri aliniatia, nilimwona na kwa bahati nzuri nilikuwa kiongozi wa kwanza Afrika kukutana yake, tulizungumza alinihakikishia miradi yote ya Serikali iliyopita fedha zake zipo na itatekelezwa."

Hivyo aliwaagiza watendaji wanaosimamia miradi hiyo ya maendeleo ikiwamo ya afya, Ukimwi na MCC kuharakisha kukamilisha tathmini za miradi hiyo, ili isichukue muda mrefu kwa ajili ya kuepuka kupanda kwa gharama wakati wa utekelezaji wake.

"Kwa kuwa fedha za miradi hii zipo, ni muhimu sana wahusika wanaosimamia miradi wasichukue muda mrefu zaidi ili utekelezaji wake uanze mara moja kwa manufaa ya Watanzania," alisema Rais.

Awali, Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoa wa Morogoro, Makoye Ng'erere, alisema mradi wa kufikisha umeme kutoka Pangawe hadi Mkuyuni na Mkuyuni hadi Matombo, utagharimu jumla ya Sh bilioni 2.8 katika utekelezaji wa awamu mbili zitakazokwenda kwa pamoja unaotarajiwa kuanza Mei mwakani.

Katika hatua nyingine, Meneja huyo alisema kiasi cha Sh milioni 89 zimetengwa na Tanesco ili kusambaza umeme katika mji wa Gairo na shule ya sekondari Sekwao ambayo alizinduliwa na Rais Kikwete.